Kura ya Maoni ya Sauti ya Waaboriginal na Wanavisiwa wa Torres Strait kwa Bunge

Watu wa Australia wanatoka nchi nyingi, wakifuata imani nyingi na kuzungumza lugha nyingi. Mataifa ya Waaboriginal na Wanavisiwa wa Torres Strait ni Watu wa Kwanza wa Australia na wameishi hapa kwa zaidi ya miaka 65,000. Lakini Katiba ya Australia haitambui hadhi yao ya kipekee. Hiyo ndiyo sababu baadaye mwaka huu, tutaweza kufikiri mabadiliko ya Katiba yetu kupitia Kura ya Maoni. Waaustralia wote watapata nafasi kutambua haki ya Mataifa ya Waaboriginal na Wanavisiwa wa Torres Strait katika Katiba yetu kupitia Sauti ambayo itahakikisha wanasikilizwa kuhusu masuala yanayowahusu.

Kauli ya Uluru kutoka Moyoni (Uluru Statement from the Heart) ni nini?

Katika Mei 2017, zaidi ya watu 250 Waaboriginal na Wanavisiwa wa Torres Strait walitoa Kauli ya Uluru kutoka Moyoni. Kauli hii hutuomba tuunde mustakabali bora kwa Australia yote na kujumuisha Sauti ya Waaboriginal na Wanavisiwa wa Torres Strait kwenye Katiba ya Australia.

Sauti ya Waaboriginal na Wanavisiwa wa Torres Strait ni nini?

Sauti ya Waaboriginal na Wanavisiwa wa Torres Strait ni njia ya mataifa ya Waaboriginal na Wanavisiwa wa Torres Strait kuishauri Serikali kuhusu sheria na sera ambazo zinawahusu.

Kura ya Maoni ni nini?

Kura ya maoni hutokea wakati wapigaji kura wanapoulizwa kujibu Ndiyo au Hapana kwa swali au maswali. Njia pekee ya kubadilisha Katiba ya Australia ni kupitia Kura ya maoni.

Nani anaweza kupiga kura katika Kura ya Maoni?

Watu pekee ambao wamejiandikisha kupiga kura wanaweza kushiriki katika Kura ya Maoni. Kupiga kura katika Kura ya Maoni ni lazima kwa wapigaji kura walioandikisha.

Je, nitapiga kura vipi katika Kura ya Maoni?

Kura za maoni ni kama uchaguzi. Siku ya kupiga kura, unaweza kwenda mahali pa kupigia kura na kupiga kura yako kwenye karatasi ya kupigia kura.

Kura ya Maoni huamuliwa vipi??

Ili Kura ya Maoni kuwa na mafanikio, inahitaji kura nyingi mbili. Inamaanisha kura nyingi katika angalau majimbo manne pamoja na kote Australia.

Je, Kura ya Maoni ya Sauti ya Waaboriginal na Wanavisiwa wa Torres Strait itafanyika lini?

Kura ya Maoni ya Sauti ya Waaboriginal na Wanavisiwa wa Torres Strait itafanyika baadaye mwaka huu.

Kura ya Maoni ya Sauti ya Waaboriginal na Wanavisiwa wa Torres Strait itauliza swali ipi?

“Sheria Iliyopendekezwa: kubadilisha Katiba ili kutambua Watu wa Kwanza wa Australia kwa kuanzisha Sauti ya Waaboriginal na Wanavisiwa wa Torres Strait. Je, unakubali mabadiliko yaliyopendekezwa?”

Ni akina nani waliunda karatasi hii ya habari?

Karatasi hii ya ukweli iliundwa na juhudi za pamoja za Life Without Barriers, Reconciliation Australia, SNAICC – National Voice for our children, Yes Alliance na Polaron Language Services. Ushirikiano huu uliundwa ili kusaidia kuunda taarifa zinazoweza kufikiwa kuhusu Sauti ya Waaboriginal na Wanavisiwa wa Torres Strait.

Ninaweza kupata habari zaidi wapi?

The National Indigenous Australians Agency www.niaa.gov.au
SNAICC National Voice for our Children www.snaicc.org.au
Reconciliation Australia www.reconciliation.org.au
First Peoples Disability Network www.fpdn.org.au
Life Without Barriers www.lwb.org.au
Yes 23 www.yes23.com.au
Polaron www.polaron.com.au
Have Your Say www.haveyoursay.net